

# **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI  
NA MAWASILIANO**



**MAMLAKA YA MAWASILIANO  
TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

## **UKIUKWAJI WA KANUNI ZA UTANGAZAJI ULIOFANYWA NA CLOUDS TV PAMOJA NA CLOUDS FM RADIO**

### **MUHTASARI**

Mnamo tarehe 10 Julai 2010 na 14 Julai 2016 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni kwa Clouds Entertainment FM Radio na Clouds Television kwa ajili ya kutoa maudhui ya Utangazaji.

Mnamo tarehe 26 Agosti 2020 kati ya saa 01:00 hadi saa 04:00 asubuhi kupitia vipindi vya Clouds 360 na cha Power Breakfast vya Clouds TV na Clouds Radio, Clouds vilirusha takwimu za wagombea wa Ubunge waliopita bila kupingwa, huku taarifa hiyo ikiwa haijathibitishwa na Tume ya Uchaguzi na kukosa mizania.

Mtangazaji alisikika akisema:

***“Sasa kuna wagombea ambao wamepita bila kupingwa...mimi nilikuwa nazo 23 mpaka saa hizi (kumi na nane zikaongezekaje hizo zingine)...si watu wanazidi ku-confirm (kwa hiyo kuna uwezekano kwamba zinaweza kuzidi)...zinaweza kuzidi...”***

***“ishapita kwasaabu, aaah mpaka saivi, mpaka tunaingia mitamboni hapa...23 washafika...”***

*Kifungu cha 16 (1) cha Kanuni za Utangazaji (Maudhui) na Kanuni Ndogo za Utangazaji (Code of Conduct) wakati wa uchaguzi za mwaka 2015 zinabainisha wajibu wa mtoa maudhui kutoa Taarifa za matokeo ya uchaguzi kwa kadri zinavyopatikana na kutolewa na Tume ya Uchaguzi na kuhakikisha matokeo yanatangazwa kwa ufasaha.*

*Kifungu cha 16 (2) cha Kanuni za Utangazaji (Maudhui) na Kanuni Ndogo za Utangazaji wakati wa uchaguzi za mwaka 2015 zinakataza mtoa huduma kutangaza maoni yatakayohamasisha vurugu au kuchochea chuki za kisiasa zinazoweza kusababisha madhara.*

*Kifungu cha 5 (j) cha Kanuni za Utangazaji (Maudhui) na (Kanuni Ndogo za Utangazaji wa Masuala ya Uchaguzi)* wakati wa uchaguzi za mwaka 2015, kinamtaka mtoa huduma kufuata maelekezo yanayotolewa na Sheria ya Uchaguzi ambapo pamoja na mambo mengine mtoa huduma atatangaza matokeo kama yatakavyotolewa na Tume.

Mtoa huduma ya maudhui anapaswa kufuata kanuni, sheria, na masharti ya leseni sambamba na maelekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

Katika vipindi hivyo *mtoa huduma alikiuka kanuni mbalimbali zikiwemo kanuni za Utangazaji (Maudhui) na Kanuni Ndogo za Utangazaji* wakati wa uchaguzi za mwaka 2015.

Mnamo tarehe 26 Agosti 2020, TCRA ilitoa Amri kwa Clouds Television na Clouds Entertainment Fm Radio ikiwataka kufika tarehe 27 Agosti 2020 kutoa maelezo kwa nini hatua za kisheria zisichukuliwe dhidi yao kwa kukiuka kifungu cha 16 (1),(2) na 5(j) cha Kanuni za Utangazaji na *Kanuni Ndogo za Utangazaji wa Masuala ya Uchaguzi* za mwaka 2015.

## **UAMUZI WA TCRA DHIDI YA CLOUDS TELEVISION**

TCRA imeamua kama ifuatavyo:-

1. Kuanzia muda wa agizo hili mpaka mwisho wa siku ya leo Clouds Television wanatakiwa kuahirisha matangazo yote na **kutumia muda wote uliobaki wa siku ya leo kuomba radhi** kwa umma wa Tanzania kwa kukiuka Kanuni za Utangazaji kupitia kipindi cha Clouds 360.
2. TCRA pia imesitisha utoaji huduma za utangazaji za Clouds Television kwa muda wa siku Saba kuanzia tarehe 28 Agosti, 2020 hadi 3 Septemba, 2020.
3. Iwapo Clouds Television itashindwa, itakataa au kukaidi Uamuzi huu, hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti zitachukuliwa dhidi ya Clouds Television.

## **UAMUZI WA TCRA DHIDI YA CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO**

TCRA imeamua kama ifuatavyo:-

1. Kuanzia muda wa agizo hili mpaka mwisho wa siku ya leo Clouds Entertainment Fm Radio wanatakiwa kuahirisha matangazo yote na **kutumia muda wote uliobaki wa siku ya leo kuomba radhi** kwa

umma wa Tanzania kwa kukiuka Kanuni za Utangazaji na Kanuni Ndogo za Utangazaji wa Masuala ya Uchaguzi za mwaka 2015 kupitia kipindi cha Clouds Entertainment Fm Radio.

2. TCRA pia imesitisha utoaji huduma za utangazaji za Clouds Entertainment Fm Radio muda wa siku Saba kuanzia tarehe 28 Agosti, 2020 hadi 3 Septemba, 2020.
3. Iwapo Clouds Entertainment Fm Radio itashindwa, itakataa au kukaidi uamuzi huu, hatua zaidi za kisheria na kuiudhibiti zitachukuliwa dhidi ya Clouds Entertainment Fm Radio

**IMETOLEWA NA  
MKURUGENZI MKUU  
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA  
27.08.2020**